


HALMASHAURI YA MJI KIBAHA



TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kibaha anatangaza nafasi kumi (10) za kazi. Maombi ya kujaza nafasi yoyote kati ya hizo yanakaribishwa kutoka kwa mtanzania yoyote mwenye sifa zilizotajwa katika tangazo hili. Nafasi zinazotanganzwa ni kama ifuatavyo:-

1. MTENDAJI WA MTAAC DARAJA LA III (NAFASI 6)

Sifa za Mwombaji

- i. Awe amehitimu Elimu ya Kidato cha Nne (IV) au Sita (VI)
- ii. Awe amehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika fani za Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya sanaa kutoka Chuo cha Serikali za mitaa Hombolo Dodoma au chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

MAJUKUMU

- i. Afisa masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Mtaa
- ii. Kusimamia ulinzi na usalama wa raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Mtaa.
- iii. Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Mtaa.
- iv. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Mtaa.
- v. Kutasfiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
- vi. Kuandaa taarifa za Utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
- vii. Kiongozi wa Wakuu wa vitengo vya kitaalam katika Mtaa.
- viii. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Mtaa.
- ix. Mwenyekiti wa kikao cha wataalamu waliopo katika mtaa.
- x. Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi.
- xi. Kusimamia utungaji wa Sheria ndogo za Mtaa.

NGAZI YA MSHAHARA TGS B.

2. DEREVA DARAJA LA II (NAFASI 4)

Sifa za Mwombaji

- i. Awe amehitimu kidato cha Nne (IV).
- ii. Awe na leseni ya Daraja la E au C1 ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali.

- iii. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha Mafunzo ya Ufundu Stadi (VETA) au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.
- iv. Wenye cheti cha Majaribio ya Ufundu Daraja la II watafikiriwa kwanza.

MAJUKUMU

- i. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
- ii. Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazo.
- iii. Kufanya matengenezo madogomadogo ya gari
- iv. Kukusanya na kusambaza nyarakaa mbalimbali.
- v. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari.
- vi. Kufanya usafi wa gari na
- vii. Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na Msimamizi wake.

NGAZI YA MSHAHARA TGS B.

VIGEZO NA MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI

- I. Mwombaji awe raia wa Tanzania
- II. Awe na umri usiozidi miaka 45 na usiopungua miaka 18.
- III. Maombi yote yaambatanishwe na nakala ya cheti cha Taaluma, nakala ya cheti cha Kidato cha nne/sita, Maelezo binafsi yanayojitosheleza (CV) ikiwa na anuani, namba za simu za kuaminika na picha mbili (passport size) za hivi karibuni (ziandikwe jina kwa nyuma)
- IV. Vyeti vyote vya Taaluma na Kidato Nne/Sita ni lazima vithibitishwe na Hakimu au wakili anayetambulika na Serikali. Aidha atakayewasilisha taarifa na sifa za kugushi atachukuliwa hatua za Kisheria na mamlaka zinazohusika
- V. Mwombaji ye yote ambaye hatazingatia mojawapo ya masharti au vigezo tajwa hapo juu, maombi yake hayatashughulikiwa
- VI. Watumishi ambao walikwisha kuajiriwa hapo awali Serikalini na kupangiwa nafasi hizo wasiombe kwa kuwa hawataweza kuingia kwenye Payroll ya Serikali.
- VII. Waombaji wote waambatanishe nakala ya cheti cha kuzaliwa
- VIII. Maombi yote yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.

Barua zote zitumwe kwa njia ya posta, maombi yatakayowasilishwa kwa mkono au barua pepe hayatafanyiwa kazi. **Barua zote zitumwe kwa njia ya posta kupitia anuani ifuatayo:-**

Mkurugenzi wa Mji,

Halmashauri ya Mji Kibaha,

S. L. P. 30112,

KIBAHA.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **07/06/2022** Saa **09.30** Alasiri.

Limetolewa na:


ENG. MSHAMU A. MUNDE
MKURUGENZI WA MJII
KIBAHA

*MKURUGENZI WA MJII
HALMASHAURI YA MUI KIBAHA*